SOCIETAS DIVINI SALVATORIS
HALMASHAURI KUU YA SHIRIKA LA WASALVATORAIAN
Via della Conciliazione, 51
00193 ROMA (Italia)
simu: +39 (06) 68629.512 baua-pepe: milton.zonta@mailsds.org

Padre Milton Zonta SDS
Mkuu wa Shirika

Itifaki AVB 20 – 072 SWA

Roma, 7 April 2020

Kwenu nyote wanachama wa Shirika la Mungu Mwokozi

Ndugu wapendwa,

Ninawasalimu nyote toka Nyumbamama hapa Roma. Ninawaandikia kwa namna ya kipekee katika Pasaka hii ambapo twasherehekea tukio la kiini cha imani yetu, yaani: mateso, kifo na ufufuko wa Yesu Mwokozi wetu, tukio ambalo kilele chake ni Pasaka. Katika kila mienendo ya liturjia ya Pasaka tunaalikwa kuwa jirani zaidi na Yesu kwa kushiriki katika Mateso yake, tuwe sehemu ya mateso hayo na kutafakari - kwa kuinua mioyo yetu -kwa fumbo la msalaba, ili kwamba pamoja naye tuweze kushinda nguvu ya kifo na kufurahia Ufufuko wake, ambamo twaweza kung'ara kwa tumaini letu la baadaye.

Kwa kweli, haliwezi kuwa Juma Kuu kama mengine ambayo tumeyasherehekea mara nyingi. Kwa dharura hii ya kimataifa kiafya, katika nchi nyingi maadhimisho ya kiliturjia ya Juma Kuu yanafanyika bila ya uwepo wa waamini kimwili. Lakini, nina hakika kwamba juu ya hali hii ngeni isiyotegemewa, wakati huu umejaa nguvu kubwa: ni mwaliko wa kuzama kwa kina katika hali hiyo ili tujiruhusu kuonja ndani mwetu mioyo idundayo ya familia nyingi ambayo huonja uchungu, kilio na maombolezo kwa vifo vya wapendwa wao. Na tujiambatanishe basi kwa ukarimu thabiti wa makumi ya mapadre, watawa wake kwa waume ambao wamekufa tokana na janga hili katili, wakibeba msalaba mabegani mwao na kutambua mchango usio na kikomo wa Yesu Mwokozi wetu. Tunaona pia undani mwingine wa kuumiza: wahanga hao wote wamezikwa bila kuagwa au ibada za mazishi! Katika uhalisia huu ambao ni mchungu, katika hali ya kuachwa na upweke sana, tunalia pamoja na Bwana wakati ule alipohisi kuwa jirani mno na kifo chake: "Mungu wangu, Mungu wangu! Mbona umeniacha?" (Mk 15:34; Mt 27:46).

Katikati ya mtikisiko huu, ningependa niwapatie vidokezo vichache vya tafakari – kwa matumizi binafsi au katika jumuiya – kwa kuanzia na kauli za Papa Fransis, ambazo zinatualika tusiogope tuwapo mbele ya shida tupaswazo kuzikabili leo katika nyakati hizi za Virusi vya Korona. Ikiwa kweli tunataka kusherehekea Pasaka, ushindi wa Uhai wetu dhidi ya kifo, ushuhuda wetu wa

Pasaka ni kuishinda hofu pale tunapokabiliana na hali za kifo, yaani kutokuruhusu hofu hizo zitutawale.

1. Awali ya yote, napenda kuwashukuru wanashirika wote wanaotafuta namna ya kuwasaidia watu kukabiliana na wakati huu mgumu. Nimeona maadhimisho mbalimbali na mazuri kwa njia ya teknolojia za kisasa ambazo zinalisaidia Kanisa kuwa jirani na waamini na watu wanaoteseka na kufungwa. Ningependa niwashukuru wale wote wanaofikiria neno la kutia moyo na faraja kwenye muda huu wa changamoto kwa njia ya kuisoma Biblia kisala. Asanteni pia kwa juhudi za mshikamano na ujumbe uliolekezwa kwa madaktari, wahudumu wa kidini na wa kiutu ambao wanahatarisha maisha yao kuokoa maisha ya wengine. *"Tuwaombee, kwa ajili ya familia zao, na tumshukuru Mungu kwa mfano wa ujasiri wanaotupatia kwa kuwatibu wagonjwa"* (Papa Fransis). Ni lazima tukabiliane na muda huu wa changamoto kwa uvumbuzi ambao unatokana na upendo na kusikiliza Neno. Hatuwezi kuruhusu kutengwa kimwili kuhalalishwe kana kwamba ni utume uliowekwa kando.
2. Kwa kuzingatia umakini wa shida ya sasa kiulimwengu, huu ni muda wa kukua katika umoja uliotukuka. Hapa Italia, kauli-mbiu: "andra' tutto bene" (m.y. kila kitu kitakuwa sawa) imeenea kwenye mitandao ya kijamii na kwenye michoro ya watoto. Katika wakati huu wa giza, nasi kama Wasalvatorian, tubebe ujumbe wa matumaini kwa unyenyekevu kwa uzoefu mkubwa wa kupendwa na Mungu katika nyakati zote na sehemu zote. Zaidi ya hayo, katika hali hii ... *"tuko katika mashua moja, wote tepetevu na dhaifu, lakini wakati huo huo, ni muhumu na lazima, tumeitwa sote kupanga safu moja, sote tunahitaji kufarijiana"* (Papa Fransis). Na tuwe watu tunaousoma wakati huu kwa misingi ya tunu za Injili: wito wa kuunganisha nguvu, kujenga madaraja, kuwa wapanzi wa matumaini katika maisha, na kuelewa kuwa hakuna yeyote aliyeokolewa peke yake.
3. Hakuna anayeweza kubashiri ni muda gani shida hii itaisha wala athari zake kwa ulimwengu. Kwa hakika ulimwengu hautakuwa sawa kama ulivyokuwa. Hata hivyo, je, kuna litakalobadilika katika mtindo wetu wa kuishi? Kwa kweli, hatujui kwa hakika athari za kila kitu kinachoweza kutokea kiulimwengu. Hata hivyo, tulichonacho mikononi mwetu ni uwezekano wa mabadiliko yetu. Hatuwezi kwenda kwa namna hii *"kufikiria daima kuwa wenye afya kwenye ulimwengu unaougua."* (Papa Fransis). Hali hii ni mojawapo ya kutengwa kunakotutaka sisi kukua katika utambuzi: kufikiri kwa kina namna yetu ya kuishi ndani na nje, kufafanua upya vipaumbele vyetu, kukua katika uhusiano wa karibu na Yesu, kutathmini ubora wa mahusiano yetu na watu na vitu. Tujiulize: sisi watawa wake kwa waume, hatukujizamisha pia katika maradhi ya kimtazamo wa kujali sana vitu licha ya kuwa tumeweka nadhiri ya ufukara wa kiinjili?
4. Tukiwa kama viongozi wa Shirika, janga la virusi vya korona linatulazimisha kufikiri upya juu ya mipango yetu. Katika muda huu usio na uhakika kuna maswali muhimu yanayotudai *"... paji la utambuzi na sala ili tufanye vizuri."* (Papa Fransis) Janga hili litakuwa na athari zipi katika kazi zetu za kitume? Na, je, katika nyumba zetu za malezi? Vipi nako kwenye misioni zetu mpya? Ni miradi ipi ya Shirika tuipe kipaumbele? Na kazi zipi tuzisimamishe kwa muda au kuziacha? Kwa muda huu hatuna majibu bado. Hata hivyo, kwa idhini ya Halmashauri Kuu, ninapenda kuwajulisha kuwa **Muhula wa tano wa Shule ya Walezi** ambao ulipangwa kuanza Mei 3 mpaka 13 mwaka huu; **Mkutano wa Kimataifa wa Tume ya Fedha** ulipangwa kufanyika Roma mwezi Juni tarehe 9 mpaka 11 mwaka huu; na vile vile **Sinodi Kuu ya Shirika** iliyopangwa kufanyika huko Timisoara Julai

20 mpaka 30 mwaka huu 2020, **VITAAHIRISHWA**. Halmashauri Kuu itaendelea kufikiri juu ya mabadiliko haya na mengine muhimu kwa siku zijazo juu ya Shirika letu.

5. Katika nchi ambazo zimeathiriwa na ugonjwa, maadhimisho ya Juma Kuu yataangaliwa moja kwa moja kimitandao na kila mmoja akiwa nyumbani. Kwa maneno mengine, mwaka huu tutasherehekea Juma Kuu ndani katika maana halisi, tukikumbuka Mateso, Kifo na Ufufuko wa Yesu ambayo yanaendelea katika mateso na ufufuko wa utu. Na tuitanabahishe njia hii, kwamba Uzima umeshinda kifo. *"Yesu anatuletea utulivu katika dhoruba zetu kwa sababu katika Mungu uzima haufi"* (Papa Fransis). Ujumbe huu wa wokovu na ujaze nyoyo zetu na kurudisha matumaini katikati ya jaribu linaloukumbwa ulimwengu. Ningependa kuwakumbusha kuwa Tridua ya Pasaka inatuonesha kiwango ambacho upendo wa Mungu aliye Hai na wa Kweli hauishiwi nguvu na humuokoa kila mmoja. Kwa kuwa hatushauriwi kukumbatiana au kupeana mikono kama hitaji la busara ili kuimarisha kuwa mbalimbali tusiambukizane, ninawaalika: mnapopeana kheri ya Pasaka chagueni baadhi ya nyimbo za furaha ya Kipasaka na kuziimba pamoja.
6. Zaidi ya hayo, katika majuma haya nimefikiria mara nyingi kuhusu maneno ya Injili ambayo yanaongelea juu ya "nguvu ya uponyaji" kutoka kwa Yesu. "Nguvu ilikuwa inatoka ndani yake na kuwaponya wote" (Lk 6:19 na Mk 5:30). Yawezekana ni nguvu ya uponyaji huu tunayoihitaji katika saa hii ya maumivu na wasiwasi kwa wote, bila kubagua. Sisi Wasalvatorian, tuliopakwa mafuta kwa nguvu ya Roho wa Yesu Mwokozi, tumeitwa kutenda kadiri ya wito wetu, ambao ni kuiangazia nguvu ya baraka hii kubwa ambayo hutoka kwa Roho wa Mungu na ambayo tunaipokea kutoka kwa Yesu Mfufuka. Muda huu wa giza kwetu sote tunatakiwa kukuza uwezo wa kujijenga upya, kwa sababu *"ikiwa uovu huambukizwa, basi ni vizuri. Basi tujiruhusu kuambukizwa mema na kueneza mema!"* (Papa Fransis). Ningependa niwahimize kushirikishana, katika dhana ya wajibu wa kitume, bila ya kuogopa kubeba roho ya sadaka, ambayo itahitajika katika maeneo mengi. Tuendelee, bila ya kukata tamaa, tukiwa thabiti katika matumaini hata kama hakuna tena sababu ya kutumaini kwa sababu hivi ndivyo Mwanzishi wetu aliliishi hilo pia: *"Mateso yoyote yawajiapo, daima songeni mbele katika Bwana!"* (SD II/79).

Mwishoni, ningependa kumalizia kwa pendekezo kwamba tufuate hatua za kujikinga dhidi ya kuenea kwa virusi vya korona, kwa kuzingatia kikamilifu sana hali ya kila nchi husika, katika unyenyekevu na utii wa uwajibikaji kwa manufaa ya wote. Tunaweza tu kuondokana na hali hii kwa umoja. Kwa hiyo, na tuukumbatie msalaba wa wakati huu kama muda wa thamani wa kuboresha rasilimali zingine na wa fursa ambazo kwa hakika hazingelikuwepo nyakati za utulivu. Narudia, kwamba kujitenga kijamii kama sehemu ya wajibu wetu kwa ajili ya jema la wote si sababu ya kujitenga kiutume. Tukisukumwa na mapendo ya utumishi kwa tamaa kwamba kila mmoja daima amjue kwa undani Mungu aliye Hai na wa Kweli, hii na iwe saa nzuri ya kuhuisha kwa nguvu na uthabiti wito huu wa kitume. Mungu awabariki! Hatuko peke yetu katika kipindi hiki cha majaribu! Furaha yetu ni Kristo Mfufuka aliye hai na anayeishi ndani yetu. Tuombeane, tukiwa tumeungana katika imani kwa wito ule ule wa kitume!

Ninayewasalimu kidugu katika Kristo Mfufuka,

Pd. Milton Zonta SDS
Mkuu wa Shirika

SOCIETATIS DIVINI SALVATORIS + SUPERIOR GENERALIS +

Pd. Agustin Van Baelen SDS
Katibu Mkuu